# MWONGOZO WA USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MAONESHO YA NNE YA BIASHARA YA KIMATAIFA YA AFRICA (4TH INTRA AFRICAN TRADE FAIR 2025 TAREHE 4 – 10 SEPTEMBA, 2025) JIJI LA ALGIERS NCHINI ALGERIA

## 1. UTANGULIZI

Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kwa mara ya tatu inaratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya 4 ya IATF, 2025 yatakayofanyika tarehe 4 – 10 Septemba, 2025 jijini Algiers, Algeria. Maonesho haya yanategemewa kuwa na washiriki zaidi ya 2000, nchi zaidi ya 140, Watembeleaji na Wanunuzi wapatao 35,000 pia kufanya mikataba ya Biashara na Uwekezaji yenye Dola za Kimarekani Bilioni 44.

Kauli mbiu ya Maonesho ya IAFT ni **Gateway to new opportunities** ambayo inalenga kuhamasisha Washiriki na Jumuiya za Kiafrika kuhusu matumizi ya Soko huru la Africa ili kupata fursa mpya kwa Wafanyabiashara na wawekezaji kupitia Ushirikiano wa kikanda

## 2. AINA ZA USHIRIKI

Ushiriki wa Tanzania katika Maonesho haya umegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) kama ifuatavyo: -

**2.1.** Wizara/Taasisi za Umma;
**2.2.** Taasisi za Sekta Binafsi na
**2.3.** Kampuni na Wafanyabiashara

## 3. BIDHAA NA HUDUMA ZITAKAZOONYESHWA

Bidhaa zitakazooneshwa kwenye banda la Tanzania ni pamoja na bidhaa za Viwandani, Sekta ya Kilimo na Uchakataji wa Mazao, Mavazi, Ujenzi na Miundombinu, Bidhaa za Watumiaji (Consumer Goods), Sekta za Ubunifu na Burudani, Elimu, Nishati, Fedha, Afya na Madawa, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Utafiti, Ubunifu na Maendeleo, Usafirishaji na Ugavi (Logistics),Uzalishaji Viwandani (Manufacturing), Madini na Rasilimali za Madini (Mining and Minerals),Viwango na Miundombinu ya Ubora, Usafiri wa Anga na Utalii, Vijana na Biashara (Startups).

4. **MANUFAA YA USHIRIKI**

Manufaa ya ushiriki wa Tanzania katika ushiriki wa IATF, 2025 ni kama ifuatavyo:-

a. Kupata oda zenye thamani ya dola za Kimarekani zaidi 81,000
b. Kuingia makubaliano ya biashara na uwekezaji wenye thamani ya dola za Marekani milioni 150
c. Kupata wabia wa Uwekezaji katika Miradi yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 500
d. Kupata watalii milioni 2 kutoka nchi za Afrika na Mataifa
e. Kupata wanunuzi 50 wa sekta ya kilimo, madini, uvuvi, nyama
f. Kushiriki katika mikutano 6 ya biashara na uwekezaji

5. **UTARATIBU WA KUSHIRIKI KWA BANDA LA TANZANIA KATIKA IATF, 2025,**

Gharama za ushiriki ni **dola 2,000** za Kimarekani kwa Kampuni na Taasisi na **dola 1,000** kwa Wajasiriamali (SME's). Mshiriki anatakiwa kupokea mwaliko na uthitisho wa ushiriki kutoka TanTrade, mshiriki atatakiwa kubainisha malengo ya ushiriki wake, idadi ya washiriki, kuwasilisha taarifa (Wasifu) huduma zinazotolewa na Wizara/Taasisi/ Kampuni, kijigharamia malazi na chakula.

Gharama ya VISA ni USD dola za Kimarekani 50 kwa mshiriki, picha 2 (passport size with blue background) na barua ya utambulisho kutoka TAN TRADE. Mshiriki anatakiwa kulipia nauli ya ndege kwenda Nigeria na kurudi Tanzania kupitia Emirates Airways, *Qatar Airways, Turkish Airlines, Saudia, Air Algerie, Egypt Air na Air Tanzania.*

6. **SIFA ZA WASHIRIKI**

Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -

i. Awe na Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
ii. Awe na Namba ya Mlipa Kodi (TIN) kutoka TRA;
iii. Awe na Leseni na vibali hai ya kufanya biashara Kitaifa na Kimataifa;
iv. Awe na uwezo wa kufanya biashara za Kimataifa.

7. **PROGRAMU ZA TANZANIA ZITAKAZOSHIRIKI**

i. Kongamano la Biashara na Uwekezaji
ii. Mikutano ya kibiashara (B2B& B2G)
iii. Siku Maalumu (National Days)
iv. Utafiti na Ubunifu wa Afrika (Africa Research & Innovation Platform)

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na**
Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade),
S.L.P 5402,
**DAR ES SALAAM.**
**Barua pepe:** enquires@tantrade.go.tz